Uthibitisho wa kurudi shuleni/kituo cha kutunza watoto

Wazazi/Walezi,

Tafadhali jaza fomu hii ya kuthibitisha kwamba ni salama kwa mtoto wako kurudi shuleni au kwenye kituo cha kutunza watoto (shule ya msingi na ya sekondari).

Jina la mtoto: _____

Kituocha kutunza watoto/shule: _____

Mtoto wangu hakutimiza vigezo vya vipimo vya shuleni vya COVID-19 vya Ontario au alirudishwa nyumbani kutoka kwenye kituo cha kutunza watoto/shuleni
tarehe _____. Mtoto wangu anaweza kurudi kwenye kituo cha kutunza watoto/shuleni tarehe
dd/mm/yyyy
_____kwa sababu zifuatazo:
dd/mm/yyyy

Tafadhali teua kisanduku kimoja na ukumbuke kwamba ni lazima mtoto wako atimize vigezo vyote vya chaguo ulililoteua:

☐ Mtoto wangu **alipimwa na kupatikana kuwa hajaambukizwa ugonjwa wa COVID-19** baada ya kuanza kujihisi kuwa mgonjwa, **na:**

- Kwa sasa mtoto wangu hana homa (bila kutumia dawa); **na**
- Imepita angalau siku moja tangu mtoto wangu alipoanza kupata nafuu;na
- Mtoto wangu hajasafiri nje ya nchi ya Kanada, AU zimepita siku **14** tangu aliporudi nchini; **na**
- Hajatambuliwa kama mtu aliyekaribiana na mtu aliyethibitishwa au anayeshukiwa kuwa na ugonjwa wa COVID-19 na idara ya Afya ya Umma au programu ya kuarifu kuhusu mtu aliyeambukizwa ugonjwa wa COVID iliyo kwenye simu yake; **na**
- Hajaagizwa na mtoa huduma za afya au ofisa wa afya ya umma kwamba ajitenge.

☐ Mtoto wangu **hakupimwa ugonjwa wa COVID-19**, lakini:

- Mtoto wangu alichunguzwa hapo awali na daktari au muuguzi mtaalamu na nilielezwa kwamba ana ugonjwa, kama vile mizio au pumu; **na**
- Ugonjwa huo ndio unaosababisha dalili ambazo mtoto wangu anaonyesha kwa sasa; **na**
- Dalili si tofauti au si mbaya sana kuliko za kawaida; **na**
- Mtoto wangu hajasafiri nje ya nchi ya Kanada, AU zimepita siku **14** tangu aliporudi nchini; **na**
- Hajatambuliwa kama mtu aliyekaribiana na mtu aliyethibitishwa kuwa na ugonjwa wa COVID-19 na idara ya Afya ya Umma au programu ya kuarifu kuhusu mtu aliyeambukizwa ugonjwa wa COVID iliyo kwenye simu yake; **na**
- Hajaagizwa na mtoa huduma za afya au ofisa wa afya ya umma kwamba ajitenge.

☐ Mtoto wangu **hakupimwa ugonjwa wa COVID-19,** hata hivyo:

- Mtoto wangu alichunguzwa na daktari au muuguzi mtaalamu tangu alipokuwa mgonjwa; **na**
- Daktari au muuguzi mtaalamu alituelezekwamba ugonjwa wa mtoto wangu unasababishwa na ugonjwa (sababu ya kimatibabu) mwingine ambao si COVID-19; **na**
- Imepita angalau siku moja tangu mtoto wangu alipoanza kupata nafuu; **na**
- Mtoto wangu hana homa (bila kutumia dawa za kupunguza homa); **na**
- Mtoto wangu hajasafiri nje ya nchi ya Kanada, AU zimepita siku **14** tangu aliporudi nchini; **na**
- Hajatambuliwa kama mtu aliyekaribiana na mtu aliyethibitishwa kwamba ana ugonjwa wa COVID-19 na idara ya Afya ya Umma au programu ya kuarifu kuhusu mtu aliyeambukizwa ugonjwa wa COVID iliyo kwenye simu yake; **na**

• Hajaagizwa na mtoa huduma za afya au ofisa wa afya ya umma kwamba ajitenge.

☐ Mtoto wangu **hakupimwa ugonjwa wa COVID-19,** lakini:

• Zimepita siku **10** tangu tarehe ambayo mtoto wangu alianza kujihisi kuwa mgonjwa; **na**

• Kwa sasa mtoto wangu hana homa (bila kutumia dawa); **na**

• Imepita angalau siku moja tangu mtoto wangu alipoanza kupata nafuu; **na**

• Mtoto wangu hajasafiri nje ya nchi ya Kanada, AU zimepita siku **14** tangu aliporudi nchini; **na**

• Hajatambuliwa kama mtu aliyekaribiana na mtu aliyethibitishwa kwamba ana ugonjwa wa COVID-19 na idara ya Afya ya Umma au programu ya kuarifu kuhusu mtu aliyeambukizwa ugonjwa wa COVID iliyo kwenye simu yake; **na**

• Hajaagizwa na mtoa huduma za afya au ofisa wa afya ya umma kwamba ajitenge.

☐ **Kurudi Shuleni:** Mtoto wangu **ni mwanafamilia wa mtu aliyetambuliwa kwamba alikaribiana na mtu aliyeambukizwa virusi ambaye baadaye alikuwa mgonjwa** (ni lazima atimize vigezo vyote):

• Matokeo ya vipimo vya COVID-19 ya mtu aliyekaribiana na aliyeambukizwa virusi yanaonyesha kwamba hajaambukizwa; **na**

• Mtoto wangu alitimiza vigezo vya vipimo vya shuleni vya COVID-19 vya Ontario leo.

☐ **Kurudi Shuleni:** Mtoto wangu **ni mwanafamilia wa mwanafamilia mwingine aliyekuwa mgonjwa lakini ambaye hajatambuliwa kama mtu aliyekaribiana na aliyeambukizwa virusi** (ni lazima atimize vigezo vyote):

• Mwanafamilia ambaye ni mgonjwa amechunguzwa kimatibabu na kupatikana na ugonjwa mwingine; **au**

• Matokeo ya vipimo vya COVID-19 vya mwanafamilia ambaye ni mgonjwa yanaonyesha kwamba hajaambukizwa virusi; **na**

• Mtoto wangu alitimiza vigezo vya vipimo vya shuleni vya COVID-19 vya Ontario leo.

☐ **Kurudi Shuleni:** Mtoto wangu **ni mwanafamilia wa mtu ambaye alikuwa katika karantini ya lazima baada ya kusafiri nje ya nchi Kanada** (ni lazima atimize vigezo vyote):

• Zimepita angalau siku **14** tangu tarehe alipokaribiana na mwanafamilia aliyekuwa kwenye karantini ya lazima; **na**

• Mwanafamilia huyo ameruhusiwa kuondoka kwenye karantini ya lazima na idara ya Afya ya Umma; **na**

• Mtoto wangu alitimiza vigezo vya vipimo vya shuleni vya COVID-19 vya Ontario leo.

☐ **Kurudi Shuleni:** Mtoto wangu **alipimwa na kupatikana kuwa ameambukizwa ugonjwa wa COVID-19** (ni lazima atimize vigezo vyote):

• Zimepita angalau siku **10** tangu mtoto wangu alipoanza kuonyesha dalili au alipopimwa na kupatikana kuwa ameambukizwa ugonjwa wa COVID-19; **na**

• Mtoto wangu ameagizwarna idara ya Afya ya Umma kwamba ni salama kurudi shuleni au kwenye kituo cha kutunza watoto; **na**

• Imepita angalau siku moja tangu mtoto wangu alipoanza kupata nafuu; na

• Mtoto wangu hana homa (bila kutumia dawaza kupunguza homa); **na**

• Mtoto alitimiza vigezo vya vipimo vya shuleni vya COVID-19 vya Ontario leo.

☐ **Kurudi Shuleni:** Mtoto wangu **alikaribiana na mtu aliyeambukizwa ugonjwa wa COVID-19 au mtu aliye na dalili za ugonjwa wa COVID-19 ambaye hakupimwa ugonjwa wa COVID-19** (ni lazima atimize vigezo vyote):

• Zimepitaangalau siku **14** tangu tarehe alipokaribiana na mtu aliyeambukizwa virusi au mtu anayeonyesha dalili za kuambukizwa virusi ambaye hakupimwa ugonjwa wa COVID-19; **na**

• Mtoto wangu ameagizwa na idara ya Afya ya Umma kwamba ni salama kurudi shuleni au kwenye kituo cha kutunza watoto; **na**

- Mtoto wangu alitimiza vigezo vya vipimo vya shuleni vya COVID-19 vya Ontario leo.

☐ **Kurudi Shuleni Baada ya Kutumwa Nyumbani:** Mtoto wangu **alirudishwa nyumbani kutoka shuleni au kwenye kituo cha kutunza watoto na aliambiwa kwamba ajitenge hadi tutakapopata mawasiliano kutoka kwa Huduma za Afya ya Umma ya Hamilton (HPHS):**

- HPHS imemruhusu mtoto wangu kuondoka kwenye karantini na kunieleza kwambamtotowangu hakukaribianana mtu ambaye amethibitishwa kuwa ameambukizwa ugonjwa wa COVID-19; **and**
- Mtoto wangu alitimiza vigezo vya vipimo vya shuleni vya COVID-19 vya Ontario leo.

Mzazi/Mlezi Jina (chapisha):

Saini ya Mzazi/Mlezi:_____ Tarehe ya Kuweka Saini:_____

Hamilton

Hamilton-Wentworth Catholic District School Board

HWDSB

Inatumika kuanzia tarehe
5 Machi 2021